8. Ikiwa una pesa za kutosha, hakuna sababu kwa nini usiende Afrika.
9. Ungalimwona, ungemwambia nini?
10. Akitaka kupanda mlima Kilimanjaro atahitaji vifaa gani?

Ufahamu

MCHEZO WA NG'OMBE

Mimi si mwana-michezo, lakini huifurahia michezo inapochezwa. Miongoni mwa michezo mingi niliyokwisha kuiona, hakuna ulionivutia zaidi ku-liko mchezo wa ng'ombe. Niliuona mchezo huu nilipotembelea Pemba miaka michache iliyopita. Ninge kuwa na uwezo ningejifunza kuucheza mchezo huu.

Mchezo wa ng'ombe unajulikana sana na wenyeji wa Pemba. Ni mchezo waupendao mno wenyeji wa Pemba. Vitabu vya Historia vyaeleza kwamba,

asili ya mchezo wa ng'ombe ni Ureno. Ajabu iliyopo ni kule mchezo wa ng'ombe kufika Pemba na mahali ambapo ni mbali mno kutoka Ureno. Ingawa tunajua kwamba Wareno waliwahi kuzitawala pande hizi katika karne ya 16 na 17, vitabu hivi vingaliandikwa na mtu wa Pemba, vingalituambia kuwa chanzo cha mchezo huu ni hapa hapa Pemba.

Mchezo huu unaendelea kucheza hapa Pemba na huwavuta watu wa kila aina. Kama uwanja wa michezo usingekuwa mkubwa ya kutosha, watu wengi hawangeweza kuingia kuona mchezo huu uchezwapo. Siku hizi kama mtu akitaka kupata nafasi nzuri sharti awahi kiwanjani masaa mawili au matatu kabla ya mchezo kuanza.

Nilikuwa mwalimu wa shule moja ya sekondari wakati wa fursa ya kuona mchezo wa ng'ombe ilipotokeza. Ilikuwa siku ya Ijumaa, siku ambayo kazi za serikali hufupishwa na zile za kibinafsi mara nyingi huvunjwa kabisa. Matayarisho ya mchezo wenyewe yalifanywa kabla. Ng'ombe mkali alikuwa tayari kifungoni. Uwanja wa mchezo ulikwisha kung'olewa visiki, mashimo kufukiwa na vijilima kuchongwa. Madungu yaliuzunguka uwanja mzima. Ndani ya uwanja mkubwa mlikuwa na bigili. Hii ilikuwa ni sehemu ya mpiga zumari, wapiga ngoma na ya wanawake wanaopiga makofi na kuimba.



Siku hiyo nilikuwa mjini na sikutaka kurudi hotelini. Kama ningefanya hivyo, nisingewahi kwenda na kurudi kwa sababu hoteli niliyokaa ilijitenga na uwanja wa michezo kwa masafa marefu ya miguu na bahari ya kuvuka.

Ilipofika saa za mchana, wanaume, wanawake, watoto na vizee, walianza kumiminika kutoka pande zote za Mtambwe. Ililazimu kufika mapema ili mtu apate nafasi juu ya madungu. Wakati inangojwa saa ya kuanza ifike, watazamaji walitumbuizwa kwa nyimbo zilizofuatishwa kwa muziki. Saa ikafika yapata saa kumi hivi, ngo'mbe aliyekuwa si ndama wala si fahali aliyezeeka, aliingizwa uwanjani kati ya vifijo na hoi hoi. Mguu mmoja wa lile dume la ng'ombe ulikuwa umefungwa ngoweo ndefu kumzuia asitoroke. Nilianza kujjuliza moyoni ni kitu gani kitakachofanya ng'ombe huyu awe mkali hata mchezo wenyewe usisimue? Kumbe yale makofi, ng'oma iliyopigwa pamoja na mlio wa zumari ambalo lilielekezwa masikioni mwake na ghasia za wale wanawake waliokuwa ndani ya chumba kulimhamakisha yule fahali. Uso wa fahali yule ulijaa ghadhabu na macho yake aliyatupa hapa na pale kama kwamba anachagua wapi ashambulie. Naam, hakupoteza wakati, mara aliwashambulia vijana waliosimama uwanjani huku wameshika vibacha au vipande vya jamvi. Kila kijana alifanya awezavyo kumkwepa ng'ombe aliyejaa hasira. Ikawa dume yule huwaendea huku na kule kwa kutaraji atapata mtu wa kumvunja mbavu au kumtegua mguu. Ikawa kazi ni hiyo hiyo mpaka alipoingia uwanjani mzee mmoja mwenye umri upatao miaka hamsini na tano au sitini. Mzee huyu aliingizwa uwanjani kwa tamaa ya kupewa bahashishi, ilionyesha kama yule ng'ombe amefundishwa kumchagua mzee, kwani alipomshambulia tu, alimbwaga chini kama gunia la chumvi. Tulipata habari siku ya pili kuwa yule mzee aliumia sana na amelazwa hospitali yu taabani.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Kwa nini mwandishi anasema ni ajabu kwa mchezo wa ng'ombe kuwapo kisiwani Pemba?
2. Toa sababu inayowawezesha watu kuwa na nafasi ya kuutazama mchezo wa ng'ombe huko Pemba.
3. Mwandishi aliona nini wakati wa mchezo huu. Eleza kwa kifupi hatua kwa hatua.
4. Chagua maneno saba kati ya haya yafuatayo na utunge sentenzi kuonyesha matumizi yake.

karne	kisiki	ndama
fahali	bahashishi	bigili
fursa	zumari	masafa
ngoweo	vifijo	vibacha
bwaga	tegua	kutaraji

Kazi Maalum

Wanafunzi wasimulie juu ya mchezo wapendao kucheza au kutazama.

HABARI ZA SARUFI

Conditional tenses

There are different kinds of conditional tenses.

1. -ki-

ki is used to state the condition on which a further fact depends.

For example:

Akifika atamwona.

"If he comes he will see him."

-ki- states the premise, whether suppositional or real, on which the rest of the sentence depends. This use of **-ki** differs from the one we saw in the discussion of compound tenses in Lesson 10. I said in that discussion that **-ki-** is used to express a continuous or repetitive action. With that function, it appears in the main verb of a compound tense. The conditional **ki-** appears in the subordinate verb (For example, the conditional clause) of the compound tense. While the **-ki-** in Lesson 10 can be replaced by **-na-** the conditional **-ki-** cannot be replaced by **-na-** because **-na-** can only be used as a simple tense and not as a conditional tense. The conditional **-ki-** may be used with the verb "to be" **kuwa** to form a compound tense with a second verb of the conditional clause. For example:

Ikiwa atafika, nitamwona.

"If he will come, I will see him."

This is interpreted similarly to:

Akifika nitamwona.

"If he comes, I will see him."

If the verb to be is not used, **kama** may be used which interprets as "if it be". **Kama** may appear with all the conditional tenses and when it does, there is an additional emphasis on the condition of fulfilment.

2. -nge-

-nge- expresses the possibility or expectation of a fulfilment. As such it appears in both the clauses of the sentence. That is, in the condition and the consequence of the sentence.

For example:

Angefika angemwona.

"If he had come, he would see him."

3. -ngali-

-ngali- expresses a condition which was not fulfilled. Like **-nge-** it appears in both the condition and the consequence of the sentence.

For example:

Angalifika angalimwona.

"Had he come, he would have seen him."

4 nge and ngali

It is possible to combine **-ngali-** and **-nge-** to form a compound tense with the same interpretation of unfulfilled condition.

For example:

Angalikuja angemwona.

"Had he come, he would see him."

-ki- may also combine with either **-nge-** or **-ngali-** to form a compound tense. When this happens, **-ki-** appears in the auxiliary verb **wa** ('be'). Otherwise, **kama** is used.

5. -nga-

-nga- is used without **-li-** to express concession, a "though" idea.

For example:

Angafika mara kwa mara, hajaweza kuonana naye.

"Although he comes frequently, he has not had a chance to meet with him."

Ingawa u mgeni, wajua mengi kushinda wenyeji

"Although you are a foreigner, you know more than the natives."

6. -japo-

-japo- is also used to express a concession. It may be used with or without the verb **wa**. The full form is **ijapo** but the short form **japo** may also be used.

For example:

Ijapokuwa hafanyi kazi si mvivu.

"Although he does not work he is not lazy."

Ijapo/Japo mgeni anajua sheria za hapa.

"Though he is a foreigner, he knows the rules here."

Notice that both **-nga-** and **-japo-** involve the negative. This is consequential to the concessional interpretation embodied in the form.

MSAMIATI

asili	origin, tradition, ancestry, source.
bahashishi	gratuity, gift, tip (cf same as bakhishishi).
bendera	flag.
binafsi	personal, personally.
-bwaga	throw off/down, tip a load off one's shoulder.
bigili	arena.
fahali	bull.
fursa	opportunity, chance.
ghasia	confusion, bustle, disturbance.
-hamaki	be seized with a sudden temper, become suddenly vexed.
hatua	steps, measures.
jamvi	floor mat.
karne	century.
kisiki	log, stump, trunk of a fallen tree.
-kwepa	avoid, duck, avoid a blow or being hurt by something.
lazimu	compel, necessitate, oblige.
(ma)tayarisho	preparations.
(ma)shimo	pit, hole.
(ma)dungu	stage or platform raised from the ground.
mbavu	ribs.
-miminika	pour out, overflow (used of a crowd of people.)
	msamiati unaendelea

miongoni
ndama
ngoweo
-shambulia
-stahafu
taabani
tamaa
-taraji
tarajia
-tawala
-tegua
-umia
(vi)bacha
vifiyo
(wa)teja
zumari

among, amongst.
calf.
strong piece of rope.
attack.
retire from work.
seriously ill, in great distress.
longing, desire, ambition.
expect, intend, look forward to;
expect, intend.
rule, manage, govern.
let a trap off, remove a snare.
be/get hurt, feel pain.
rag, piece of cloth or floor mat.
applauses, noises of approval.
customers.
wind instrument.

SOMO LA KUMI NA MBILI

MAZOEZI MAALUM

A. Ziandike sentensi hizi kwa kutumia kiambisho -sh-

Kwa mfano:

Mwalimu alitu.....(beba) vitabu.

Mwalimu alitubebesha vitabu.

1. Mama alim.....(la) mtoto chakula.
2. Alii.....(kaa) chupa mezani.
3. Atawa.....(funga) mizigo yote ili waende nayo.
4. Bibi alim.....(lala) mtoto kitandani.
5. Nitawa.....(enda) katika motokaa yangu.
6. Baada ya kifo cha baba yake, marafiki walijaribu kuwa.....(sahau) tukio hilo.
7. Kila siku huni.....(imba) nyimbo za ku.....(cheka).
8. Nilipotaka kupita alini.....(pita) chini handakini.
9. Alipomw.....(anguka) mtoto alivunjika mguu na mkono.
10. Nguo zake zilipolowa alijaribu kuzi.....(kauka) kwa moto.
11. Atawa.....(lipa) madeni yote kwa lazima.
12. Tunataka ku.....(bahati) tikiti za mchezo huu.
13. Tulianza ku.....(tayari) vyakula vya karamu.

B. Kujenga Msamiati

1. Ukitaka kutafuta maneno haya katika kamusi, ni maneno gani hasa utakayotafuta?

amechaguliwa	niliyekuamini	walisumbuliwa
sibadilishi	aliwahuzunisha	zitatangazwa
alimpigisha	akamtambulisha	walimshuhudia
kumsikiliza	hakikai	wameshughulika
walikubaliana	akasimamishwa	kikatekwa.

2. Chagua (5) na tunga sentenzi kuonyesha maana kamili.

MICHEZO SHULENI

Ilikuwa siku ya Ijumaa katika shule ya Mwereni. Wanafunzi wote walikuwa na furaha kwa sababu ni siku ya mwisho ya juma. Wanafunzi wanaipenda sana siku hii kwa sababu nyingi. Kwanza, wanafunzi watakuwa na siku mbili za kupumzika kabla ya kuanza shule tena siku ya Jumatatu. Pili, wanafunzi hupewa nafasi ya kushiriki katika mashindano mbalimbali ya michezo kama vile, mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mbio za masafa marefu, kutupa tufe, kutupa mikuki, ndondi, na michezo mingine.

Mavumilio ni mwanafunzi katika shule ya Mwereni. Anapenda mashindano ya mbio za riadha. Mwaka wa 1984, alishiriki katika michezo ya Kimataifa ya Olimpiki huko Los Angeles, Marikani. Ingawaje hakupata medali yo yote, alifanya vizuri kiasi cha kuwapa moyo wachezaji wengine katika shule ya Mwereni. Katika mashindano ya mwaka 1988, anategemea kwenda Korea Kusini akiongozana na wanafunzi wengine kama watachaguliwa.

Siku hizi, Mavumilio hana raha hata kidogo. Amekuwa anajiandaa kwa mtihani wake wa mwisho. Kwa hivyo, hajaweza kufanya mazoezi inavyopasa ili kujiweka tayari kwa mashindano ya Korea. Siku hii ya Ijumaa ilikuwa siku ya mashindano kati ya shule ya Mwereni na shule ya Kazi Moto. Kutokana na mashindano haya, wakuu wa michezo ya riadha watafanya uchaguzi wa awali kwa watakaoshindana kitaifa kabla ya uchaguzi wa watakaoi-wakilisha Tanzania huko Korea. Alianza kusikitika na kuona kwamba ata-iaibisha shule yake na atajiaibisha mwenyewe pia. Alifikiri juu ya kukosa kushiriki katika mashindano haya. Kwa sababu alikuwa hajawahi kukosa kushiriki katika mashindano haya hata siku moja aliona ni budi ajitahidi kwa uwezo wake wote. Filimbi ya kujiandaa ilipigwa na washindani wote walijitokeza uwanjani. Mavumilio alijiona mnyonge, miguu ilikuwa haina nguvu. Alijiunga na wenzake na kungojea amri ya kuanza mashindano.

Mara alisikia "pha". Alijua hio ni alama ya kuanza kukimbia. Alitimua mbio. Alipoangalia mbele yake, aliwaona vijana watatu wamemtangulia. Alisikia mwili wote umemisimka. Alisikia pia wanafunzi wa Mwereni wakishangilia kwa nguvu. "Mavu!, Mavu!"

Aliongeza mbio. Mara akajiona amewapita washindani waliomtangulia. Aliuvuka utepe na kuwa mshindi wa kwanza. Wanafunzi wenziwe waliingia kiwanjani wakimshangilia. Walimnyanyua juu huku wakimshangilia kwa kusema "Mavu !, Mavu!, Mavu !". Alitambua kuwa ameiletea shule yake

sifa kubwa na amejweka katika orodha ya wanariadha wa mashindano ya Korea mwaka wa 1988. Alisema kimoyomoyo, "Kweli, penye nia pana njia."

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Kwa nini Mavumilio ni mhusika mkuu katika hadithi hii?
2. Ilitokea nini mwaka 1984?
3. Kwa nini siku hii ya Ijumaa ilikuwa muhimu kwa Mavumilio?
4. Kwa nini Mavumilio alikuwa na wasiwasi?
5. Mashindano yalikuwaje mwanzoni?
6. Mshindi wa kwanza alikuwa nani?
7. Kwa nini Mavumilio alisema "penye nia pana njia."?

Andika maneneo haya kwa kiingereza

-sumbua	tufe	mbio za kupokezana
-subiri	mkuki	ndondi
-amua	-wahi	-shauri

Kazi Maalum

Wanafunzi watayarisha masimulizi yenye kufafanua methali ya "penye nia pana njia." Masimulizi haya yanaweza kuonyesha tukio la kweli au hadithi ya kutungwa tu. Wanafunzi watoe masimulizi haya darasani.

HABARI ZA SARUFI

The Causative form

There are different forms to indicate the causative depending on the verb and other phonetic features. The proto-Bantu form was *ya*. In some cases it has been assimilated depending on the end consonants of the verb root. Where no assimilation has taken place, the causative suffix is either *-ish* or *-esh* following vowel harmony rules similar to those of the applied suffix. Thus:

1. Verb roots which end with *-k*, the *-k* changes to *-sh*.

For example:

ruka = rusha

anguka = angusha

exceptions:

weka = wekesha

fika = fikisha

2. Verb roots which end in a vowel take **-z**. For example:
kataa → kataza
ingia → ingiza
3. Verbs of non-Bantu origin take **-ish**, **-esh** depending on vowel harmony. For example:
rudi → rudisha
sahau → sahaulisha
samehe → samehesha
4. Verbs made from nouns, adjectives, and adverbs (especially of Arabic origin) take **-ish** or **-esh** depending on vowel harmony. For example:
bahati → bahatisha
tayari → tayarisha
5. There are some irregulars depending on the Swahili community one is in contact with. Most second language speakers of Swahili will use the second alternative.
fanya → fanyiza/fanyisha
penda → pendeza/pendesha
ogopa → ogofya/ogopesha
nawa → navya/nawisha

The causative form is used to express causation. Caution should be exercised when translations are made because the interpretation of causation in Swahili does not always match that of English on a one to one basis. In Swahili causation may be used to cover such concepts as persuasion, permission, compulsion and the general simple idea of cause.

For example:

- (a) persuasion: **bembeleza** 'comfort'
- (b) permission: **kopesha** 'lend'
- (c) compulsion: **kimbiza** 'chase', 'cause to run'

For some forms, it is difficult to decide which category to put them.

For example:

- uguza** 'tend a sick person'
pigisha chapa 'print a book'

For these, the interpretation lies largely on the context. Certain causative forms may include an "intensive" interpretation.

For example:

- tokeza** 'come forth', 'emerge'.
angaza 'shine brightly'.

Grammatically the object of the causative verb is the agent of the action. The subject of the verb makes it possible for the action to take place.

MSAMIATI

-amini	trust, believe, have confidence.
-amua	decide, make up ones mind.
-amulia	decide for.
-andaa	prepare.
awali	initial, first, foremost.
filimbi	whistle.
handaki	an underground tunnel.
-jitahidi	make effort, try very hard.
-jitokeza	emerge, be outstanding.
kimoyomoyo	by heart; whisper to oneself.
kutupa tufe	throwing disk.
kutupa mkuki	throwing spear(javelin).
-lowa	get wet.
mbio za riadha	sprint.
medali	medal.
(m)shindi	winner.
(m)nyonge	a weak person.
nanga	anchor.
nia	intention.
-nyanyua	lift up.
-ongozana	accompanying, be in a group of.
-pa moyo	encourage.
-pasa	require, oblige.
-shangilia	cheer, make rejoicings, applaud.
shauri	matter, plan, advice, consideration.
-shauri	give counsel, advise, (kata shauri decide.)
-sikitika	be sad.

-shuhudia	witness.
-sisimka	be excited, make the blood race.
-sumbua	disturb, annoy, cause discomfort.
-tambua	recognize, realize.
-tangulia	precede, advance.
-tegemea	expect.
-teka	capture, take/take up, carry off.
-timua	take off fast.
tukio	a happening, an event (usually sudden, unexpected).
uchaguzi	selection, choice.
utepe	ribbon.
-unga	join, accompany.
uwezo	ability.
-vuka	cross over.
-wahi	having a chance, have a chance to do something.
-wakilisha	represent.
(wa)shindani	competitors.



MAZOEZI MAALUM

A. Andika kwa kukanusha

1. Simama pale.
2. Mtoto ninayemtafuta alipotea jana.
3. Nenda dukani ukanunue maziwa ya chai na sukari.
4. Mwambie dada yako mgeni wako aitwaje.
5. Waulizeni wazazi kama watakuja kwa ndege au kwa miguu.
6. Mtu anayekujua anaweza kukuharibia maisha yako.
7. Tuleteeni chai na mikate tafadhali.

B. Ziandike sentenzi hizi kwa kutumia -ik- au -ek-

Kwa mfano:

- (a) Kamba hiyo ita.....(kata)
 - (b) Kamba hiyo itakatika.
1. Mlango ume.....(fungua) wenyewe.
 2. Kitabu hiki kina.....(soma)? Mbona maandishi yake ni madogo sana.
 3. Afadhali watoto hawa wana.....(fundisha).
 4. Mambo kama haya ni rahisi sana ku.....(sahau).
 5. Yeye ame.....(bahati) kuingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
 6. Anapenda ku.....(shughuli) sana. Kila mara yu safarini.
 7. Ame.....(tajiri) kwa urithi wa baba yake.
 8. Maua haya ya.....(pendeza) machoni.
 9. Visiki hivi vya.....(ngo'a) kwa urahisi sana.
 10. Sauti ili.....(sikia) kwa mbali kama mtoto aliaye kwa uchungu.

C. Sasa zitafsiri sentenzi 1-10 kwa Kiingereza

Ufahamu

UKOSEFU WA MAJI VIJIJINI

Viongozi wengi wa Afrika wafahamu vema kwamba zaidi ya jamii mia moja katika vijiji mbalimbali hulazimika kusafiri zaidi ya maili moja ili kupata maji safi ya kunywa. Wengine hutegemea maji ya visima au maji ya bomba, lakini wakati wa kiangazi, visima na bomba hukauka.

Serikali kwa muda mwingi imehusika sana na hali hii, na sasa imeamua kuwafanyia wananchi shime ya kupata maji. Serikali inafanya mipango kuleta maji ya bomba vijijini na kuongeza idadi ya visima vya maji. Hata hivyo ni gharama kubwa na shida zinaongezeka kwa sababu ya idadi ya watu kuwa kubwa mno katika vijiji. Sasa hata mijini kuna shida ya maji katika sehemu mbalimbali za Afrika. Matatizo haya hayawezi kutatuliwa kwa kutegemea misaada ya nchi za nje. Ni budi wananchi wenyewe wavumbue njia rahisi za kutatua matatizo haya bila ya kugharimu kiasi kikubwa cha fedha za serikali.

Mipango inayofaa ni kama kuviunganisha vijito vilivyopo nchini na kuongeza idadi ya maji yaendayo mkondo mmoja. Maji haya yatakusanywa katika bwawa kubwa na kuhifadhiwa vizuri. Mpango mwingine, ni kuangalia matumizi ya maji. Wakati wa kiangazi, wananchi washauriwe kutumia maji kwa uangalifu. Wapunguze shughuli za umwagiliaji maji isipokuwa mahali pa lazima. Wananchi wahimizwe kulima mazao yasiyohitaji maji mengi na pia waoteshe mimea ya kivuli kuzuia kupotea kwa unyevu unyevu katika ardhini uletwao na mvua kubwa za masika.

Si watu wengi watakaofaidika na mipango hii mwanzoni, lakini ikikamilika yote, kazi ambayo itachukua muda wa miaka miwili au zaidi, itasaidia sana kwa kuleta maendeleo ya kudumu katika sehemu mbalimbali za Afrika. Baada ya muda si mrefu, sehemu nyingi zitaweza kujitegemea kwa matumizi ya maji na mazao ya chakula ili kupunguza tatizo la njaa. Kwa hivyo kufaulu au kutofaulu kwa mipango hii kutawategemea wananchi wenyewe. Kama watafanya bidii na kufanya kazi kwa moyo mmoja, taabu hizi zitakwisha bila shaka. Sehemu itakayofanikiwa itakuwa mfano kwa sehemu nyingine za nchi, Afrika na hata dunia nzima.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Ili kupata maji safi ya kunywa, wanavijiji wanalazimika kufanya nini?

2. Wakati wa shida kubwa ya maji vijijini ni wakati gani? Kwa nini?
3. Serikali za nchi za Afrika zinafanya nini kutatua tatizo hili la maji?
4. Ili kutatua tatizo hili, ni budi wananchi wafanye nini?
5. Taja mipango ambayo inafaa kufanywa.
6. Kama mipango hii itafanikiwa, kutakuwa na faida gani?

Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu ulichosoma

lazimika	shime	mkondo
kauka	bomba	vumbua
amua	husika	gharimu
otesha	kudumu	fanikiwa

Andika sentenzi nzuri ukitumia maneno haya

fanya shime	umwagiliaji maji	faidika
himiza	wavumbue	matatizo

Kazi Maalum

Wanafunzi wachague nchi moja katika nchi zinazoendelea. Wafanye utafiti kuhusu usambazaji wa huduma maalum na kuandika insha juu yake. Insha hii inaweza kusomwa darasani na mwanafunzi mwenyewe.

HABARI ZA SARUFI

The Stative (also called neuter) form

1. The stative extension is indicated by **-ek** or **-ik** following the necessary vowel harmony rules.
For example:
soma → **somika** 'readable'.
pika → **pikika** 'cookable'.
penda → **pendeka** 'likable', 'lovable'.
ng'oa → **ng'oleka** 'uprootable'
2. For verbs that have been extended by the causative form **-ik-** or **-ek-** is used. For example:
fundisha → **fundishika**
pendeza → **pendezeka**
3. Verbs of non-Bantu origin add **-(1)ika**, **-(1)eka** depending on the verb morphology.

For example:

rudi → **rudika**

samehe → **sameheka**

sahau → **sahaulika**

4. It is possible to form stative verbs from nouns, adjectives, or adverbs by adding **-ka**.

For example:

shughuli → **shughulika**

bahati → **bahatika**

tajiri → **tajirika**

Note that the stative is not expressed by the form **-ka** only. Some verbs are inherently stative without the **-ka** form.

For example:

tazama 'look at'

nyamaa 'be silent'

andama(na) 'follow (each other)'

kaa 'stay', 'sit'

The primary function of the stative marker is to express a state. In addition it expresses potentiality (i.e. the capability to happen or to be fulfilled). Generally, a stative verb takes the tense marker **me**. But when expressing potentiality it may take other tenses and also the **na** of association.

For example:

pata → **patikana** 'obtainable'

weza → **wezekana** 'possible'

MSAMIATI

dam.

pipe.

of necessity, no escape, no way out.

lasting.

profit, benefit.

be successful.

cost, expense, price.

cf. gharama, (to) cost .

protect, provide sanctuary.

urge.

be involved.

dry up.

a tree stump.

shade, shadow.

problems, hardships, inconveniences.

wailing.

current, flow, rush, passage.

scatter, spread, distribute.

collect.

used as an appeal for collective effort.

solve (lit. tear).

act of pouring (cf. mwaga).

distribution.

dampness.

well.

discover, find by chance.

prevent.

bwawa
bomba
budi
-dumu
-faidika
-fanikiwa
gharama
-gharimu
-hifadhi
-himiza
-husika
-kauka
kisiki
kivuli
(ma)tatizo
mayowe
mkondo
-sambaa/sambaza
-sanya
shime
-tatu
umwagiliaji
usambazaji
unyevu
(vi)sima
vumbua
-zuia

SOMO LA KUMI NA NNE

MAZOEZI MAALUM

A. Chagua sentenzi iliyo sahihi kati ya zifuatazo

- 1a. Alikuwa nilikuwa ninasoma.
- b. Alikuwa nilipokuwa nikisoma.
- c. Alikuwa nilipokuwa nilisoma.
- 2a. Nimeona vile wewe unafanya.
- b. Nimekuona unafanya.
- c. Nimekuona vile unavyofanya.
- 3a. Niliambia yeye asichelewe.
- b. Nilimwambia asichelewe.
- c. Nilimwambia kuwa yeye asichelewe.
- 4a. Kichwa kinaniuma
- b. Kichwa kinauma mimi.
- c. Kichwa changu kinauma mimi.
- 5a. Utakata kidole chako.
- b. Utajikata kidole chako.
- c. Utakikata kidole chako.
- 6a. Tulishindwa kufungua ule mlango.
- b. Hatujaweza kufungua mlango ule.
- c. Hatujaweza kuufungua mlango ule.
- 7a. Samaki waliwekwa chumbani ya barafu.
- b. Samaki ziliwekwa chumbani mwa barafu.
- c. Samaki waliwekwa katika chumba cha barafu.
- 8a. Wamo watu wawili garini.
- b. Kuna watu wawili ndani ya gari.
- c. Watu wawili ni ndani ya gari.
- 9a. Zawadi hizi watapewa washindi wote.
- b. Zawadi hizi zitawapewa washindi wote.
- c. Zawadi hizi zitapewa kwa washindi wote.
- 10a. Dirisha hali wazi.
- b. Dirisha haliko wazi.
- c. Dirisha si wazi.

B. Chagua neno moja na jaza nafasi hizi.

1. Mama aliporudi nyumbani alikuwa amebeba
faru, mtungi, nyumba, motokaa.
2. Zainabu ana mazoea ya kula chakula bila
kunawa, hanawi, ananawa, hakunawa.
3. Nilisahau kumrudishia viatu
zake, yake, lake, vyake.
4. Alipowasili, alikaribishwa vyema kwa
fujo, vifjo, kelele, matata.
5. Kazi ya mpishi ni nzuri isiyo na
ngumu, faida, kifani, maana.
6. Licha ya kuwa yeye ni mwizi na mnyang'anyi, ni
mkorofi, mkongwe, mtaratibu, mwema.
7. Pesa zangu zimo
paani, mezani, mvunguni, mfukoni.
8. ni mseja.
baba yangu, mama yangu, dada yangu, kaka yangu.
9. Alipozirai
alizungumza vizuri, alitaka chakula, alifunga macho, aliomba msamaha.
10. Kwa sababu aliumia mguu, aliondoka kiwanjani
akichechemea, akitimka, akiruka ruka, akitambaa.

C. Badilisha sentenzi hizi kwa kutumia wakati uजा

1. Jana nililala saa sita.
2. Nimemwambia aje kuniona.
3. Suzana ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Stanford.
4. Viti alivyonunua ni vizuri lakini ni ghali sana.
5. Sikununua mananasi yo yote mwaka jana.
6. Mwanafunzi huyo amekwenda kwao.
7. Walipofika karibu na bandari waliona nyumba za wenyeji.
8. Nchi zinazopata uhuru sasa zina shida kubwa za kiuchumi.
9. Kuna mashindano ya mpira leo jioni.
10. Aliyefika ni mwanae, si yeye mzee.

Ufahamu

MUUNDO WA MASHAIRI

Katika somo la nane, tulisoma juu ya uandishi wa mashairi. Tulisoma juu ya beti, vina, kituo, na mizani. Tulisoma shairi juu ya ukulima. Tuliona kwamba lugha ya ushairi si lugha ya kawaida kama watumiavyo watu wanapozungumza. Mshairi anaweza kulazimika kupunguza au kuongeza silabi katika maneno anayotumia. Kwa mfano shairi la Ukulima, ubeti wa kwanza, mstari wa kwanza, mwandishi anatumia neno **zindukana**. badala ya **zinduka**. Hapa mwandishi ameongeza silabi moja ili kuwa na mizani ya kutosha kwa mstari huo. Pia mwandishi hatumii mnyambuliko wa vitenzi kama tutumiavyo wakati wa kuzungumza. Kwa mfano, mwandishi anaweza kusema "wengi tafaidika" badala ya "wengi watafaidika". Kwa kulisoma shairi kwa makini, unaweza kuona baadhi ya maneno ambayo mwandishi amegeuza mnyambuliko wake ili kuzingatia kanuni bora za uandishi wa mashairi.

Yafuatayo ni mashairi machache mafupi ambayo tutayasoma na kuona jinsi mwandishi anavyoitumia lugha katika ushairi.

Shairi la Kwanza

KIPI BORA?

Enyi ndugu mashuhuri, bado sijahakikisha
Ningali ninafikiri, kichwa chanigonganisha
Wenzangu wakashairi, mawazo yanikondesha
Chakula, hewa, na maji, Kipi ni bora zaidi

Mwenzangu nahangaika, swali linavyotingisha
Vitu vitatu hakika, kweli vinaniangusha
Wananchi wasifika, shime kunisalimisha
Chakula, hewa, na maji, Kipi ni bora zaidi

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo

1. Shairi hili ni juu ya nini?
2. Ni maneno gani ambayo mshairi amebadilisha mnyambuliko wake ili kuzingatia kanuni za uandishi wa mashairi. Ameyabadilishaje?

3. Kwa kutumia maneno yako mwenyewe, eleza anayosema mshairi wa shairi hili.

Shairi la Pili

MAPATANO

Japo sikuhdhuria, wa Arusha mkutano.
Ndevu nilifurahia, yale maafikiano.
Kwa Kenya na Somalia, kuunganisha mkono.
Yadumishe mapatano, ya Kenya na Somalia.

Ulikuwa ni udhia, tena ni aibu mno.
Nchi zilizo huria, kuanzisha farakano.
Mipaka mwaigombia, pasi na masikizano.
Yadumishe mapatano, ya Kenya na Somalia.

Majuzi walipokea, kwenye majadiliano .
Kaunda kajitolea, yarejeshwe mapatano.
Kwani ndugu wakilia, jirani hali vinono .
Yadumishwe mapatano, ya Kenya na Somalia .

Zikafikiwa hatua, za kushikana mikono.
Egal wa Somalia, Kenyatta wa Kenya ino.
Meza moja wakakaa, kwamba mwisho wa mapigano.
Yadumishwe mapatano, ya Kenya na Somalia.

MASWALI YA UFAHAMU


Jibu maswali yafuatayo

1. Unafikiri mshairi alikuwako katika mkutano wa Arusha?
2. Mapatano anayozungumzia mshairi ni kati ya nani na nani?
3. Kwa nini mwandishi anasema ni "aibu"?
4. Nchi azungumziawo mwandishi, zilipatana baada ya mkutano? Andika mstari wa shairi unaohibitisha jibu lako.
5. Mstari wa mwisho ni kiini au ni kituo cha shairi.
6. Vipange vina vya shairi hili kama vinavyoonyeshwa katika shairi.
7. Tafuta maneno ambayo mshairi amebadilisha mnyambuliko wake ili kuzingatia idadi ya mizani. Onyesha alivyobadilisha.

8. Katika mazungumzo ya kawaida, msemaji angesemaje mawazo ya ubeti wa tatu wa shairi hili.

Kazi Maalum

Baada ya kusoma mashairi haya, wanafunzi waandike shairi fupi (beti 3 hadi 5) juu ya jambo lo lote, kwa mfano, siasa, mapenzi, maonyo, masomo, na kadhalika.



MSAMIATI

aibu	shame.
-angusha	cause to fall, drop.
baadhi	some, among.
-dumisha	cause to last, uphold, make permanent.
-faidika	profit from, be advantageous (<i>cf. faida = profit</i>).
farakano	estrangement, separation, unpleasant departure.
-geuza	change, alter.
ghali	expensive.
-gonga	knock, hit hard, hammer at.
-gomba	quarrel with, wrangle, gainsay, squabble.
hakikisha	find out the truth, confirm on the truth.
-hangaika	be troubled, be in turmoil, confused, anxious.
-hudhuria	attend, be present at a gathering.
huria	free, independent (<i>cf. huru</i>).
-jitolea	volunteer oneself.
-konda	grow thin, become lean, be emaciated.
(ma)jadiliano	discussion, debate.
makini	strength of character, dignity, serenity, intelligent.
(ma)nanasi	pineapple(s).
(ma)onyo	warning, advice.
(ma)patano	agreement, reconciliation, terms.
(ma)pigano	(<i>cf. pigana</i>) fight, battle.
mashuhuri	famous, outstanding.
(m)nyambuliko	conjugation.
(m)paka	border, division, frontier.
(m)seja	bachelor.
(ma)sikizano	agreement after a discussion.
ndevu	beard.
-nyambua	pull in pieces, conjugate.
-ongeza	increase, make more, add.
-punguza	reduce, make less.
-rejesha	cause to return, bring back to normal.
-salimisha	cause to be safe, make safe, save.
-tingisha	shake violently, cause a vibration.
udhia	annoyance.
(vi)nono	(lit. that which is fat) favourable, suitable, pleasing.
-zingatia	take into account/consideration, include in.
-zirai	faint, swoon, lose consciousness.

SOMO LA KUMI NA TANO

MAZOEZI MAALUM

A. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia mojawapo ya viungo hivi. Usitumie kiungo zaidi ya mara moja

lakini	bali	ila
pia	tena	licha ya hayo
wala	kwa sababu	kwamba
iwapo	na	halafu
kwa hivyo	kama	ingawa
kabla ya		

1. sijui kama nitapata pesa za kutosha, ninaandaa safari, huenda pakatokea bahati nikaweza kwenda.
2. Mto hauvukiki kwa daraja.
3. Hawafahamu Kiswahili lugha yao ya kwanza.
4. watafika mapema, tutaenda kutazama sinema.
5. Leta vyombo vyote masanduku yake.
6. Sitaki kula chakula chenu..... kunywa vinywaji vyenu.
7. Walisema watatupelekea majina mengine.
8. Walipewa adhabu, walionywa wasirudie tena.
9. Kwanza tutengeneze mashini hii,tuiweke katika motokaa ile.
10. Si kweli kwamba hakumwona. Alimwona mara mbili akamwambia ulivyosema.
11. Hakunipigia simu alifika mwenyewe.
12. Najua kutumia mashine hii sijui kuitumia mashine ya IBM.
13. Nilikuwa nimechoka sana.niliona ni bora nirudi nyumbani nipumzike kidogo kuanza shughuli hii.
14. Lazima tuwalipewametuokoa.
15. Andrea ni mtu mwenye bidii. Mchana kutwa hushinda ofisini, huwafundisha watu wazima jioni kwa masaa mawili au matatu.

B. Zitafsiri sentensi (1-15) ulizokamilisha hapo juu kwa Kiingereza

Ufahamu

HUDUMA ZA AFYA KISIWANI UNGUJA

Katika nchi nyingi za Afrika, matibabu yanaweza kuangaliwa katika nyakati tatu tofauti kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, na baada ya uhuru.

Kabla ya kuja kwa Wazungu, maradhi yote yalitibiwa kienyeji. Kuliwa na waganga ambao walikuwa wakitumia mizizi, magome na majani ya miti. Sayansi yao haikuwa ikijulikana, kwa hiyo, haikuwa na uchunguzi wa magonjwa wala madawa. Ili kuyatambua maradhi, mganga alipiga ramli au alipandisha pepo wa mgonjwa kichwani kusudi amfichulie siri ya ugonjwa na dawa itakayofaa. Kuna maradhi yaliyotibiwa kwa pungo pamoja na nyungu, na kupewa chano shetani. Kuna maradhi yaliyotibiwa kwa makombe ya aya za Kurani na hirizi za kuvaa mwilini. Kuna wagonjwa waliotibiwa kwa dawa za kujipikia, kunywa, na kuogea. Pia wapo wagonjwa waliotaapishwa, kuchanjwa au kufukizwa mafusho. Kidonda kilitibiwa kwa chokaa iliyochanganywa na majani ya mbono. Homa kali ilitibiwa kwa mafusho yenye mchanganyiko wa vitu kama majani ya vitunguu thomu, mavi ya tembo, majani makavu ya miti mbalimbali yenye harufu kali. Mgonjwa wa masikio alitiwa tuwi lililochanganywa na kitunguu thomo. Mgonjwa wa macho alitiwa urojo uliokamuliwa kutoka majani ya mfuu. Matibabu ya aina hii yalitegemea zaidi kubahatisha pamoja na imani ya mgonjwa kuwa atapona kuliko utafiti wa kisayansi kama tuujuavyo siku hizi. Wagonjwa wachache walipona, wengine walikufa.

Wamisionari walipofika walikuja kwa nia ya kutayarisha makao ya ukoloni. Wao walianzisha matibabu ya kulingana na sayansi yao kila walipoweka makao. Mnamo mwaka 1926, Serikali ya Kikoloni ilianzisha hospitali huko Zanzibar. Wenyeji waliita hospitali hii, "Hospitali ya Mnazi Mmoja." Kuanzishwa kwa hospitali hiyo hakukutosheleza huduma za afya. Ingawa hospitali zilizoongezwa zote zilionekana katika miji tu. Huko Pemba, Miji ya Wete, Chake Chake na Mkoani ndizo sehemu zilizobahatika kupatiwa hospitali. Vijiji vichache tu kama vile Mkokotoni, Mfenesini, na Makunduchi vilipatiwa zahanati. Ingawa katika miaka ya karibu ya Uhuru kulikuwa na Zahanati za watu binafsi, nazo pia zilikuwa mjini. Wakulima ambao hutegemea katika nchi zote changa, walipata shida kufuatia vituo vya afya masafa marefu.

Huduma za afya zilianza kuenea baada ya uhuru wa watu wa Unguja. Hatua ya kwanza iliyochukuliwa na serikali mpya ni kutangaza matibabu yasiyo malipo. Haukupita muda mrefu, serikali ya kimapinduzi ilitangaza

mpango wa kuwapatia wanavijiji zahanati huko vijijini kwao. Kwa njia ya ujenzi wa taifa pamoja na misaada ya serikali zahanati kadhaa zilijengwa visiwani mote. Zahanati hizo zilipatiwa waangalizi na wakunga wa kulala hapo hapo. Juu ya yote, kuna magari makubwa yenye zana kamili, madak-tari, na wasaidizi ambao huzitembelea zahanati za Unguja na Pemba mara kwa mara, kusudi kuendeleza huduma za afya.

Hatua ya mwisho, ambayo pia ni muhimu kama zile nilizokwisha kuzitaja ni kule kuzipanua, kuzitengeneza na kuzifanyia mabadiliko hospitali walizojenga wakoloni. Isitoshe, kuna maafisa wa afya wanaozuru vijiji ili kutoa nasaha juu ya afya bora. Radio na televisheni pia husaidia kuwasiliana na wananchi kuhusu umuhimu wa kinga kwa maradhi kama kipindupindu. Mbali ya hayo, huhimiza kukimbilia hospitali hata kwa ishara ndogo ya ugonjwa na pia kuonya hasara za kudharau kinga pamoja na tiba.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali haya

1. Kabla ya kuja kwa wakoloni, huduma za matibabu ya magonjwa zilitolewa na nani?
2. Taja njia mbali mbali zilizotumiwa ili kujaribu kutibu wagonjwa.
3. Njia hizi zilifanikiwa kuwasaidia wagonjwa? Kwa nini?
4. Ni nani walioanzisha hospitali huko Zanzibar?
5. Huduma za hospitali zilitosheleza sehemu zote Kisiwani? Kwa nini?
6. Serikali ya mapinduzi inafanya nini kuenea huduma za afya?

Kujenga msamiati

Tumia maneno haya katika sentenzi kuonyesha maana kamili

matibabu	maradhi	waganga
kuchanjwa	mchanganyiko	utafiti
wamisionari	kutosheleza	zahanati
daktari	kupanua	mbali ya hayo

Kazi Maalum

Wanafunzi wasimulie juu ya huduma za afya katika nchi yao.

Conjunctions

Conjunctions fall into two categories. Coordinating and subordinating conjunctions. Coordinating conjunctions include:

1. Those that introduce additional information.

na 'and', **pia** 'also', **tena** 'also.'

2. Those that express a choice.

ama....ama 'either...or', **au** 'or', **wala** 'neither.'

Ama atakuja ama atakwenda kumwona shangazi yake.

"He will either come or go to see his aunt."

Atasafiri leo au kesho. "He will travel today or tomorrow."

Hatakuja wala hatakwenda kumwona shangazi yake.

"He will neither come nor go to see his aunt."

Notice that, unlike its English counterpart, **wala** involves negative marking on the verb.

3. Those that express contrast.

lakini 'but', **ila** 'but', **bali** 'but rather'.

4. Those that express inference or reason.

kwa hivyo 'so', **kwa sababu** 'because, 'for the reason of', **kwa ajili ya** 'because of', 'for the reason that', 'for that matter'

Subordinating conjunctions appear in subordinate clauses. They include:

1. Those that express purpose.

ili 'so that'

2. Those that express a condition.

kama 'if', **kwamba** 'that'.

aya
-bahatisha
-chanja
chano

-dharau
-endelea
hasara

-himiza
-fukiza
hirizi

harufu
hatua
huduma

imani
ishara
kadhaa
kali

-kamua
kavu
(ki)donda

-kinga
kurani
-lingana

(ma)afisa
(ma)badiliko
(ma)fusho

(ma)gome
(ma)kao
(ma)kombe

(ma)lipo
(ma)pinduzi

verse, paragraph.

take a chance, try ones luck, cause to be lucky.

make an incision, cut into, vaccinate.

a flat round wooden platter with a low rim.

used for serving food.

ignore, despise, scorn, slight, treat with contempt, insult.

continue, proceed.

loss, misfortune.

hasten, speed up.

burn incense, cause to give smoke.

charm, amulate.

a smell, odour, scent.

measures, steps.

services.

faith.

sign, a mark, an indication.

various, several.

sharp, strong, fierce, severe, bitter.

squeeze out, wring, compress.

dry.

an ulcer, a wound.

protect, shield, defend, screen against.

Koran.

be equal, equalize, be the same, alike.

officers, officials.

change(s).

something to be burnt as a charm, or medicine.

bark of a tree, animal shell.

place of abode, quarters, headquarters, home.

treatment given by a traditional doctor by writing

verses from the Koran which is then washed off and the

water drunk by the patient. Also used to mean

a vessel, big mugs.

payment, salary.

revolution.

masafa	measure of distance, wave length.
(ma)radhi	disease in general, sickness.
(ma)tibabu	cure.
mavi	dung, excrement.
(m)changanyiko	mixture.
mbono	castor oil plant.
(m)fuu	the dead, corpse.
(m)koa	region, state, province.
mnamo	at about.
misionari	missionary.
(mi)zizi	root(s).
nasaha	advice.
nyungu	big cooking pot.
-oga	take a bath, shower.
-panua	open wide.
pungo	the ceremony of exorcism.
ramli	soothsaying from figures in sand, fortune telling.
shetani	devil, evil spirit.
-simulia	narrate, tell in a story.
siri	secret.
-taapika	vomit, be sick.
-taja	mention, list, announce.
-tangaza	announce, make public, publicize.
tembo	elephant.
thomo	garlic.
tiba	medical, associated with cure and medicine.
-tibu	treat to cure.
-tosha	be sufficient, enough, adequate.
tuwi	milky liquid got by grating coconut.
urojo	a thick mixture.
ukoloni	colonialism.
(vi)tunguu	onions.
(wa)angalizi	caretaker, supervisor.
(wa)kunga	midwife.
zahanati	dispensary, a health center.
zuru	make a special visit to a place or someone.
zana	apparatus, gadgets, munitions, fittings.

MAZOEZI MAALUM

A. Andika sentensi hizi kuwa wingi

1. Nakijua nikipendacho mwenyewe.
2. Ameibiwa jembe lake leo.
3. Huyu ndiye mtoto aliyependwa zaidi kuliko mimi.
4. Meli ilitia nanga katika bahari ya Hindi.
5. Humjui mtu huyu hata kidogo.
6. Kama unakijua kitu hiki, mbona husemi hivyo.
7. Mzee wake alimtumainia yeye siku zote lakini hakumsaidia.
8. Kiziwi humtazama msemaji usoni ili aisome midomo yake asemapo.
9. Nasema naye kila siku kabla ya kwenda kazini.
10. Ajua nisemayo lakini ajifanya hasikii.

B. Jaza nafasi kwa kutumia maneno haya

nilishuhudia	nimsindikize	alipogunduliwa
ikipepea	wakiranda randa	ustahimilivu
kufumba na kufumbua	alirejea	akamnasih
kumbembeleza	kunong'ona	

1. Kwa kuwa nilikuwapo, mambo yote yaliyotokea.
2. Kwa kuwa dada anaogopa giza, aliniomba nje kuchukua viatu vyake alivyoviacha karibu na kiwanya cha mpira.
3. Mgeni kutoka Mombasa saa kumi jioni hivi.
4. Kama kuna upepo, bendera inaweza kuonekana
5. Tulifikiri simba ameondoka. Tuliteremka juu ya miti na kuanza safari yetu tena., alitokea tena na kuanza kutukimbiza.
6. Mtoto alikuwa amelala usingizi. Ili wasimwamshe, wazazi wake walisema kwa
7. Alifikiri mambo yake ya wizi yalikuwa siri mpaka
8. Wamama wanahitaji mwingi wakati wa kulea watoto.
9. Walikuwa hawana kazi nyingi kwa hivyo saa za mchana unaweza kuwaona mjini bila kitu maalum cha kufanya.
10. Matilda alipopoteza hereni zake za dhahabu, alianza kulia kwa sauti kubwa. Ndipo dada yake na akimwambia kuwa watatafuta fedha na kununua nyingine.

AJALI HAINA KINGA

Watu waliokuwapo pwani walimshuhudia nahodha Kibuyu na rafiki zake wakiingia mashuani. Muda si muda, chombo chake kikatekwa na hapo hapo kikapata upepo wa kaskazi kukisindikiza. Kufumba na kufumbua kikawa kimeshika kasi kuelekea baharini.

Asubuhi ya siku ya tatu, Kibuyu karejea na kilio bandarini. Aliwahuzunisha hata wale waliomzunguka kumsikiliza.

"Ebu, nyamaza kwanza utueleze." Walimnasihi na kumbembeleza.

Mwishowe baada ya kwikwi na duku duku la kilio kumpungua, akaanza kusumulia: Tulikusudia kwenda Fungu Mbaraka kukaa dago kwa muda wa wiki nzima. Ilikuwa tuvua na tupige ndege lakini wapi!"

Kumaliza kusema hivyo Kibuyu akalia tena.

"Ati, Fungu Mbaraka ndiyo nini?" Kijana mmoja aliuliza kwa kunong'ona wakati watu wengine wakiwa wameshughulika kumnyamazisha Kibuyu.

"Ni kisiwa kidogo ambacho kwa desturi hakikai watu. Ni maarufu kwa ndege wake walio wengi, mchanga mweupe na usafi wa maji ya pwani yenye kuzunguka kisiwa, hicho. Tena kipo baina ya Ras mbili - Kizimkazi kwa upande wa Unguja na Kimbiji kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa mara ya mwanzo, kisiwa hicho kiligunduliwa mnamo mwaka 1758. Miaka mia moja na arobaini baadaye, serikali ya Zanzibar ilipeleka watu kukikalia kwa muda wa miezi sita. Kitendo hicho kilifanyika mnamo mwaka 1898. Tokea hapo, bendera ya Zanzibar ikawa inapepea kisiwani humo. Alieleza mzee mmoja katika kumjibu yule kijana aliyeuliza suala.

Baada ya kutulizana kidogo Kibuyu akaendelea: "Mchana wa siku ya pili, tulikwenda pwani Fungu Mbaraka. Tulitia nanga pahala pamoja tulipodhani patakuwa na samaki wengi.

Kumbe, maji safi yakisaidiwa na mwanga wa jua kali la mchana, yalifichua kila kitu. Kule chini tulipotupa nanga, samaki walikuwa wengi, walipigizana mbio kama watoto wadogo wachezao foliti. Mizia na mikiki, walionekana wakiranda randa kwa marefu na mapana. Ajabu! Juu ya wingi huo wote, hapakutokea hata samaki mmoja aliyejaribu kudonoa mishipi yetu.

Kwa kukosa ustahimilivu, Kikoti akaanza kunung'unika, "Mambo gani hayo hata samaki wanafanya majivuno!"

Mara, Kidanzi aliyekaa kwa utulivu kwenye staha ya mbele ya mashua akaita kwa hamu: "Njooi, njooi!" Kufumba na kufumbua, Kikoti akawa amekwisha kufika.

"Tazama unaona pango lile. Sijui mna nini lakini samaki wote wanaminika mle". Kidanzi alionyesha kwa kidole chake cha shahada kilichokuwa kimeng'oka ukucha.

"Lo! watanitambua." Alisema Kikoti huku akikimbilia kuchukua bunduki yake na kupiga samaki. Nilimsihi atulie kwanza, lakini hakunisikia.

Muda si muda, akawa amesha valia miwani na viatu vyake vya kupigia mbizi, na mkononi ameshika bunduki. Tahamaki dakika moja baadaye amechupa majini! Tuliacha kila kitu ikawa tunamtazama akiingia mle pangoni, lakini hakutoka tena. Tulimngojea, tukamgoja lakini wapi! Laiti angalisikia maneno yangu angalikuwa hapa anakunywa pombe nasi.

Nahodha Kibuyu alimaliza hadithi yake huku machozi yakimwaika.

MASWALI YA UFAHAMU

Jibu maswali haya

1. Kichwa cha hadithi hii ni mfano wa methali. Nini maana ya methali hii?
2. Kibuyu alikuwa nani katika hadithi hii?
3. Nani aliyepotea katika bahari? Alipoteaje?
4. Unajua nini juu ya Fungu Mbaraka.
5. Hadithi hii ni ya huzuni au ni ya kushangaza? Toa sababu zako.

Kazi Maalum

Wanafunzi wasimulie juu ya ajali waikumbukayo.

HABARI ZA SARUFI

Interjections

Interjections are forms like the following:
ati, ebu, kumbe, lo, laiti.

These interjections have a specific English translation. However, they have a specific semantic function in Swahili discourse.

1. **ati** 'by the way' is used to attract the attention of the hearer (the person being spoken to) as well as to seek confirmation on what has just been said. It may also be used in case of exhortation.
2. **ebu** 'let' is used only to attract the hearer's attention. When used, the hearer stops whatever activity is in progress and devotes total attention to the speaker.
3. **kumbe** 'so it is' is used to imply that one did not expect the information being given.
4. **lo** 'oh' is used to show a strong feeling which is agreeable or disagreeable.
5. **laiti** 'if only' is used as an expression of regret or even simple surprise.

Other forms include:

6. **naam** 'I hear you', 'acknowledged'. Depending on intonation, one knows whether the form expresses consent or whether it expresses a request by the respondent to the speaker to repeat the proposition.
7. **ewee/ewaa, ewallah** 'agreed', 'absolutely'. This form is used to express consent. It has an inferior superior conotation. That is, it shows consent from an inferior towards a superior.
